#WeweNdoFuture #TimizaWajibu

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo No. 12

October - Disemba 2023



# PROFESA MKENDA

## AHIMIZA UBORA ELIMU YA JUU

Na Mwandishi wetu
Dar es salaam

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amewataka wadhibiti ubora wa elimu Barani Afrika kuhakikisha wanafunzi wanaojiunga na masomo ya elimu ya juu wanakuwa na sifa stahiki ili kukidhi viwango vya kimataifa.

Prof. Mkenda ameyasema hayo Novemba 28, 2023, Jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa mtandao wa wadhibiti ubora wa elimu ya juu Barani Afrika (AfriQAN) uliolenga kujadili mchango wa wadhibiti ubora katika wa elimu ya juu katika dunia ya kidijitali.

Kwa mujibu wa Waziri Mkenda, wadhibiti ubora wana jukumu kubwa la kuhakikisha suala la ubora wa elimu linapewa kipaumbele kwa kuangalia maslahi mapana ya Bara la Afrika lengo likiwa kutengeneza wanataaluma na siyo wahitimu.

"Wadhibiti ubora mna kila sababu ya kuendelea kusimamia suala la ubora wa elimu. Msikubali kuangukia kwenye shinikizo la kushusha ubora kwani kuna kazi kubwa ya ufundishaji wa vyuo vikuu! Jambo muhimu ni kuhakikisha mwanafunzi anafanya vizuri" amesisitiza Prof. Mkenda.

Aidha, kuhusu kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika vyuo vikuu Prof. Mkenda ametanabaisha kuwa suala hilo linapaswa kuangaliwa kwa umakini kutokana na kasi ya ongezeko kuwa kubwa na akaongeza kuwa jambo hilo halipaswi kuwa kikwazo katika utoaji wa elimu bora au kuwazuia wahadhiri kufanya tafiti zinazolenga kupata maarifa mapya.

Awali akizungumza katika kongamano hilo, Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) Prof. Charles Kihampa amesema ushirikiano wa taasisi za udhibiti wa ubora wa elimu Barani Afrika unalenga kuhakikisha viwango vya elimu ya juu katika nchi wanachama vinawiana.

"Mtandao unatuwezesha kushirikiana na wadhibiti ubora kutoka nchi mbalimbali katika kutimiza jukumu la kudhibiti ubora wa elimu na kutuwezesha kuandaa taratibu za uendeshaji taasisi za elimu ya juu", amesema Prof. Kihampa.

Mkutano huo wa siku tatu umefanyika nchini kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa mtandao huo miaka 14 iliyopita na kujumuisha nchi 22 kutoka Afrika; Kenya, Rwanda, Uganda, Malawi, Lesotho, Eswatini, Ghana, Zambia, Niger, Nigeria, Senegal, Zimbabwe, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Cape Verde, Mali, Namibia, Angola, Ivory Coast, Misri na mwenyeji Tanzania.

Wanafunzi wanaodahiliwa katika vyuo vikuu nchini ni sehemu muhimu katika upangaji na utoaji wa mikopo ya elimu ya juu ambapo HESLB hupanga mikopo kwa takribani 70% ya wanafunzi wanaopata udahili kila mwaka.

## JAMBO LETU



Jacqueline Msuya
*Mhariri*

# Tumia mfumo kurejesha mkopo popote

Tumefika mwisho wa mwaka kwa kufunga kalenda ya mwaka 2023 na kujongea mwaka mpya wa 2024 tukiwa na shauku ya kutathmini tuliyopanga na kuyatimiza kwa mwaka 2023 na pia kufanyia kazi mafunzo tuliyoyapata kutokana na kutokamilika kwa baadhi ya mambo kama ilivyotarajiwa.

Wanasema kupanga ni kuchagua na kuchagua maana yake ni kuweka vipaumbele kwa mambo muhimu na kuyapa muda na nafasi ya kwanza. Kwa upande wa HESLB moja ya suala kubwa tulilolipanga na kulikamilisha ndani ya mwaka 2023 lilikuwa kuboresha mifumo yetu ya urejeshaji mikopo iliyoiva ya wanafunzi wa elimu ya juu ili kuwawezesha wanufaika wanaorejesha mikopo yao waweze kuifikia na kuitumia kwa urahisi zaidi mahali popote.

Kama itakumbukwa, tangu kuanza kutumika kwa mifumo ya urejeshaji wa mikopo kwa mtandao mwaka 2020 kwa mnufaika mmoja-mmoja uitwao Loanee Individual Payment Account kwa kifupi LIPA na kwa waajiri unaitwa Employer's Portal kwa kifupi EPO, wanufaika na waajiri wamepata nafuu kubwa ya kuwasiliana na HESLB ili kufikisha taarifa za waajiriwa wapya walionufaika na mikopo ya elimu ya juu na pia kuwasilisha makato kwa haraka zaidi kuliko miaka ya nyuma.

Pamoja na kuwepo kwa mifumo, tumekuwa tukitathmini ufanisi wa mifumo hiyo na kuona umuhimu wa kuboresha zaidi ili kumwezesha mteja wetu kutumia muda mfupi zaidi kupata taarifa anayohitaji kwa ajili kufanya malipo au kwa rejea yake binafsi.

Awali mnufaika na mwajiri walikuwa wanatumia namba ya kumbukumbu ya malipo ambayo ilikuwa ni lazima itengenezwe na maafisa wa HESLB kabla ya mhusika kuweza kuendelea na malipo lakini sasa kwa utaratibu mpya ulioanzishwa mwaka huu 2023 baada ya kuboresha mifumo, mwajiri au mnufaika wanaweza kutengeneza kumbukumbu ya malipo wao wenyewe wanapohitaji kufanya malipo na namba hiyo inaweza kutumika ndani ya siku 30 kwa kiasi cha fedha kilichosajiliwa kulipwa kwa wakati huo.

Jambo la muhimu kwa mnufaika ambaye hajaanza kurejesha mkopo wake bila shaka itakuwa ni jinsi anavyoweza kupata ankara yake kuona kiasi anachodaiwa, kujua jinsi atakavyolipa na njia itakayotumika kufanya malipo ya mkopo wake.

Kwa kifupi ikiwa wewe ni mnufaika utapaswa kuingia kwenye tovuti ya HESLB www.heslb.go.tz na kubofya kipengele cha 'Repay Loan' kisha bofya 'Beneficiary' ambapo utakuta uwanja wa kujaza taarifa zako zinazohitajika ukianza na namba yako ya Kidato cha Nne na mwaka uliomaliza. Baada ya kukamilisha usajili na kutengeneza nywila yako, utaweza kuingia kama mtumiaji uliyesajiliwa na kisha kujaza jina la chuo ulichosoma na taarifa za mwajiri iwapo umeajiriwa katika mfumo rasmi.

Heri ya Sikukuu ya
**KRISMASI & MWAKA MPYA**
**2024**

## NDANI...



**03**
**PROFESA MDOE:**
Vyuo viweke mazingira rafiki kwa maafisa mikopo



**04**
**SHAKIRA:**
Ahsante Rais Samia

**BODI YA UHARIRI**

**Mwenyekiti**
Abdul-Razaq Badru

**Katibu**
Omega Ngole

**Mhariri**
Jacqueline Msuya

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Eline Maronga
Jonathan Nkwabi

**Designer**
+255 736 190 083

**Mawasiliano**
Jengo la PSSSF,
Barabara ya Makole,
eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma

**Simu:**
+255 758 067577
+255 739 067577

**Barua pepe:**
dodoma@heslb.go.tz

**Tovuti:**
www.heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE



# Mifumo inarahisisha kutoa na kupokea huduma

Nakukaribisha kwa mara nyingine katika Jarida hili la mtandao ili uweze kusoma na kujua yaliyojiri katika eneo hili la ugharimiaji wa elimu ya juu hapa nchini katika robo ya pili ya mwaka 2023/2024.

Katika toleo hili la 12 tumejikita zaidi katika kuhamashisha matumizi ya TEHAMA hususan katika urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi ili kuongeza urahisi kwa wanufaika wa mikopo na ufanisi kwa upande wa utendaji wa kila siku wa HESLB katika ukusanyaji wa mikopo iliyoiva.

Mfumo wa urejeshaji mikopo unawapa fursa wanufaika na waajiri kusajili taarifa zao mtandaoni na kisha kufikia taarifa hizo kwa urahisi kila mwezi ili kurejesha makato ya mikopo yao au kupata ankara (Loan Statement) kuweza kuona makato na salio la mkopo wa mnufaika.

Ni takriban muongo mmoja sasa tangu HESLB ilipoamua kupunguza taratibu matumizi makubwa ya karatasi katika utendaji wake wa majukumu ya kila siku na kuanzisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA. Utendaji wa HESLB unamaanisha shughuli za utoaji wa mikopo, usimamizi wa urejeshaji, utunzaji wa kumbukumbu na michakato yote ya shughuli za ofisi.

Uamuzi wa ku-tehamisha shughuli za kiutendaji siyo tu umepunguza gharama za ununuzi wa karatasi lakini pia umewezesha wanufaika ambao madeni yao yameiva pia kupunguza muda na gharama za kusafiri hadi zilipo ofisi za HESLB ili kupata huduma. Hivi sasa wanufaika wanaweza kupata taarifa za madeni yao mahali popote na muda wowote na hivyo pia kuwa rahisi kulipa mahali popote kwa kutumia njia za malipo zilizorahisishwa kwa mitando ya simu au kupitia taasisi za kifedha zikiwemo benki.

Urahisi huu wa taratibu za malipo umeiwezesha HESLB kuwafikia wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu walio wengi ndani na nje ya nchi kwa wakati mmoja na kukusanya madeni kwa haraka na kwa kiwango kikubwa zaidi ukilinganisha na ilivyokuwa kwa miaka nane (08) iliyopita. Hii imewezesha pia mwenendo wa ukusanyaji wa madeni yaliyoiva kukua kutoka wastani wa TZS 2.3 bilioni kwa mwezi mwaka 2015/2016 hadi wastani wa TZS 15 bilioni kwa mwezi mwaka 2022/2023.

Pamoja na kutumia TEHAMA kwa kiasi kikubwa katika urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, kila mara tunafikiria na kuongeza ufanisi zaidi wa mifumo hiyo kutokana na kukua kwa kasi kwa teknolojia na pia kubadilika kwa mahitaji ya wadau.

HESLB kwa kutambua nafasi na thamani ya kila mdau kwenye eneo hili la ugharimiaji wa elimu ya juu, inakukaribisha pia kutoa maoni pale ambapo unahisi yatasaidia kuboresha zaidi ili sote tuweze kunufaika katika kutoa na kupokea huduma kwa urahisi, haraka na ufanisi mkubwa.

> *Utendaji wa HESLB unamaanisha shughuli za utoaji wa mikopo, usimamizi wa urejeshaji, utunzaji wa kumbukumbu na michakato yote ya shughuli za ofisi.*

# PROFESA MDOE



## Vyuo viweke mazingira rafiki kwa maafisa mikopo

*Viongozi wa taasisi za elimu ya juu wanapaswa kuunda mazingira rafiki kwa maafisa mikopo kwa kutoa vitendea kazi vinavyohitajika na mafunzo ya mara kwa mara ili kuboresha utendaji wao na utoaji wa huduma kwa wanafunzi. ... wakati taasisi hizi ni muhimu kwa maendeleo ya ujuzi kwa wanafunzi, wastani wa mapato yao 60-70% yanatokana na mikopo ya wanafunzi kupitia ada za masomo zilizolipiwa na serikali alisisitiza Prof. Mdoe.*

Na Mwandishi Wetu
Dar es Salaam

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. James Mdoe amewataka maafisa wanaosimamia madawati ya mikopo katika taasisi mbalimbali za elimu ya juu nchini kutoa huduma bora kwa wanafunzi.

Prof. Mdoe ametoa wito huo Oktoba 11, 2023 wakati akifungua kikao kazi cha siku tatu kilichofanyika mjini Bagamoyo mkoani Pwani kati ya Menejimenti ya HESLB na maafisa mikopo zaidi ya 100 kutoka taasisi 80 za kitaaluma zenye wanafunzi wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu.

"Napenda kuweka jambo hili wazi kabisa, huduma tunayowapa wanafunzi wa elimu ya juu wanaopokea mikopo siyo hisani, ni haki yao. Ninaamini kuwa mnatoa huduma nzuri na pia mnatambua kuwa mna nafasi ya kufanya vizuri zaidi kwa kuboresha utoaji wa huduma yenu …" amesema Prof. Mdoe.

Mbali na wito kwa maafisa wa mikopo, Prof. Mdoe ametoa wito kwa Uongozi wa taasisi za elimu ya juu kuimarisha ofisi za mikopo ya wanafunzi kuteua maafisa mikopo wenye uwezo na kuwawezesha kwa rasilimali ambazo zitawawezesha kutoa huduma nzuri kwa wanafunzi.

"Viongozi wa taasisi za elimu ya juu wanapaswa kuunda mazingira rafiki kwa maafisa mikopo kwa kutoa vitendea kazi vinavyohitajika na mafunzo ya mara kwa mara ili kuboresha utendaji wao na utoaji wa huduma kwa wanafunzi. ... wakati taasisi hizi ni muhimu kwa maendeleo ya ujuzi kwa wanafunzi, wastani wa mapato yao 60-70% yanatokana na mikopo ya wanafunzi kupitia ada za masomo zilizolipiwa na serikali" alisisitiza Prof. Mdoe.

Katika hotuba yake ya kumkaribisha mgeni rasmi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa HESLB, Prof. Hamisi Dihenga, alibainisha kuwa kila mwaka kabla ya kuanza kwa mwaka wa masomo, imekuwa ni desturi ya HESLB kuandaa kikao kazi cha pamoja na maafisa mikopo kwa madhumuni ya kubadilishana uzoefu.

Awali kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB Prof. Hamisi Dihenga amesema HESLB imekuwa na utaratibu wa kuandaa kikao kazi na maafisa mikopo kabla ya kuanza kwa mwaka mpya wa masomo kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kujengeana uwezo katika kutoa huduma bora kwa wanafunzi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Abdul-Razaq Badru amesema kikao kazi hicho kilichoongozwa na kauli mbiu isemayo 'Umuhimu wa TEHAMA katika kuboresha huduma kwa wanafunzi' ikilenga kuwafundisha maafisa mikopo kuhusu mifumo ya TEHAMA ya HESLB iliyoboreshwa kwa ufanisi wa mikopo ya wanafunzi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Maafisa Mikopo hao, Frida Malya ambaye pia ni Afisa Mikopo wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), aliwakumbusha wanafunzi wanaonufaika na mikopo kufuata taratibu wanapokuwa vyuoni ili kuwezesha kupata huduma bora kwa wakati.

# SHAKIRA:

## AHSANTE RAIS SAMIA



Na Mwandishi Wetu
Morogoro

Shakira Hamisi Idana, mwanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Shahada ya Utalii katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), ndaki ya Mazimbu, mwenye ulemavu wa miguu, ameishukuru serikali kwa kutoa kipaumbele katika kuwafadhili wanafunzi wenye ulemavu waweze kusoma elimu ya juu.
Shakira alizaliwa mwaka 2002 mkoani Ruvuma akiwa hana ulemavu wowote, lakini baadae mwaka 2012 alipata tatizo kwenye uti wa mgongo linalohusiana na ugonjwa wa kifua kikuu (TB ya mifupa), hali ambayo imemsababishia ulemavu wa miguu hadi leo.

"Nilipokuwa darasa la nne nilipata tatizo kwenye uti wa mgongo na ikasababisha kusitisha masomo yangu kwa mwaka mmoja, maana nilikuwa siwezi kutembea wala kukaa... Nilipatiwa dawa na kufanya mazoezi katika hospitali ya Peramiho ambayo yalinisaidia nikaweza kukaa na mwaka 2013 nilipopata nafuu, nikamuomba mama anirudishe shule na kurudia darasa la nne katika shule ya msingi Mfaranyaki iliyopo Songea," anaelezea Shakira.

Shakira ni mtoto wa kwanza katika familia ya watoto wanne inayolelewa na mama tu kwa kuwa baba yake Shakira alishafariki. Mama Shakira anafanya vibarua vya usafi kwenye nyumba za watu na kufua, ambapo kipato anachopata ndicho anatumia kuitunza familia yake.

"Namshukuru sana mama yangu kwa kujitoa kwake ili mimi niweze kusoma…nilipopata nafuu na kurudi shule, mama alikuwa akinibeba kila siku kunipeleka shule na kunirudisha nyumbani hadi nilipoweza kuanza kutembea mwenyewe na magongo," anasimulia Shakira.

Shakira alihitimu na kufaulu vizuri shule ya Msingi, hivyo akajiunga na shule ya Sekondari ya kutwa ya Mfaranyaki iliyopo Songea na kusoma kidato cha kwanza hadi cha nne. "…nilipohitimu kidato cha nne, nilifaulu na kupangiwa kwenda Mbeya katika shule ya Sekondari Kafundo ambayo ni shule ya bweni na nilifanikiwa kupata daraja la pili katika matokeo yangu ya kidato cha sita…" anaelezea Shakira.

Kuhusu uamuzi wa kusomea Shahada ya Utalii, Shakira anaamini kwenye masomo yake kuna vitu vingi vya kujifunza ambavyo vinaweza kumsaidia kujiajiri baadae. "Napenda kukutana na watu wa nchi nyingine na kuwaelezea kuhusu utajiri wa Tanzania ... lakini pia katika kozi hii ya utalii kuna masomo yanayohusiana na "Hotel Management" ambayo naamini yatanisaidia kuweza kujiajiri…" anafafanua Shakira.


Shakira anaishukuru serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kumwezesha kuendelea na masomo ya chuo kikuu akibainisha kuwa bila msaada huo asingeweza kusoma. "Naiomba Serikali iendelee kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kutimiza ndoto zao kwa kuwapa mikopo ya kutosha ili wasipate changamoto wanapokuwa chuoni. Pesa hii ya kujikimu inanisaidia kwenye chakula, malazi na matibabu…" anafafanua Shakira.

Shakira anatoa wito kwa wanafunzi wenzake waliopo vyuoni, kutumia vizuri mikopo wanayopatiwa na Serikali kusoma kwa juhudi ili wafaulu vizuri na baadae waweze kuajiriwa au kujiajiri na kuweza kurejesha mikopo waliyopatiwa iwanufaishe watanzania wengine.

**...nilipohitimu kidato cha nne, nilifaulu na kupangiwa kwenda Mbeya katika shule ya Sekondari Kafundo ambayo ni shule ya bweni na nilifanikiwa kupata daraja la pili katika matokeo yangu ya kidato cha sita... anaelezea Shakira.**




**Oktoba 4,2023, Dar es salaam:** *Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda (wa pili kushoto) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Mwongozo wa Uombaji Mikopo kwa Wanafunzi wa Stashahada kwa mwaka 2023/2024. Wa pili kulia ni Mkurugenzi wa HESLB Abdul-Razaq Badru.*



**Oktoba 9, 2023, Dar es salaam:** *Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi HESLB, Prof. Hamisi Dihenga (aliyesimama katikati mstari wa kwanza) akiwa na wajumbe wa Bodi mpya ya HESLB (2023-2026) kabla ya kuanza kwa mafunzo mafupi kwa wajumbe wapya wa Bodi katika Hoteli ya Protea Dar es salaam Courtyard.*




**Oktoba 11,2023, Bagamoyo:** *Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. James Mdoe (aliyekaa katikati) akiwa katika picha ya kumbukumbu na Menejimenti ya HESLB ikiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Prof. Hamisi Dihenga (wa pili kulia) na Maafisa Mikopo wa vyuo vya elimu ya juu vilivyopo katika Kanda ya Dodoma baada ya ufunguzi wa kikao kazi kilichofanyika Bagamoyo mkoani Pwani.*



**Oktoba 26, 2023, Dar es salaam:** *Mkurugenzi wa HESLB Abdul-Razaq Badru akizungumza na wahariri wa vyombo vya Habari (hawapo pichani) katika mkutano uliofanyika katika ukumbi wa PSSSF Golden Jubilee.*




**Oktoba 26, 2023, Dar es salaam:** *Baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya HESLB na Wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari wakimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru (hayupo pichani) wakati akiwasilisha mada katika mkutano ulioratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa PSSSF Golden Jubilee.*




**Novemba 27, 2023, Dar es salaam:** *Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB Prof. Hamisi Dihenga (mwenye shati jeupe) akipokea zawadi ya 'Zanzibar Door' kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (ZHELB) Prof. Mohammed Hafidh Khalfan (Kushoto) baada ya ziara ya kikazi katika ofisi za HESLB. Wa pili kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB Dkt. Rukkaya Muhammed.*



**Disemba 11, 2023, Dar es salaam:** *Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Mhe. Sabiha Filfil Thani (katikati) akiwa na wajumbe wa Kamati katika picha ya pamoja na Menjimenti ya HESLB ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Abdul Razaq- Badru (wa pili kulia) wakati wa ziara ya kikazi ya Kamati hiyo katika ofisi za HESLB.*




# 'WAMEJIFICHUA' WENYEWE

Na Mwandishi Wetu
Dar es Salaam

Kampeni ya 'Fichua' imeanza kushika kasi kwa wanufaika maarufu na wenye ushawishi katika jamii walioko katika sekta binafsi kuanza kujitokeza na kulipa madeni ya mikopo yao ya elimu ya juu.

Hatua ya wanufaika hao ambao waligharimiwa na Serikali kupata elimu ya juu kujitokeza na kulipa madeni ya mikopo yao inadhihirisha uzalendo na kiu waliyonayo ya kuona vijana wengine wa kitanzania nao wananufaika kama wao ili kufikia malengo yao.

Mnamo Novemba 9, 2023 alijitokeza mwandishi maarufu wa vitabu na mhamasishaji wa masuala ya stadi za maisha na uchumi, Joel Nanauka ambaye alilipa kwa mkupuo mmoja deni lake lote la elimu ya juu, kiasi cha TZS 2,928,293.38.

Siku ya Ijumaa, Novemba 10, 2023 alijitokeza mshereheshaji wa viwango vya kimataifa, Anthony Luvanda maarufu kama MC Luvanda na kulipa deni lake lote alilokuwa amekopeshwa na serikali kupitia HESLB, kiasi cha TZS 3,132,000.00, kwa mkupuo mmoja.

Katika mahojiano mafupi na HESLB YAKO, kila mmoja kwa wakati wake; Nanauka na MC Luvanda wameelezea umuhimu wa HESLB kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa wanufaika ambao madeni yao yameiva lakini bado hawajaanza kurejesha, wajitokeze ili waanze kulipa mikopo hiyo kwa njia rahisi na za kisasa zilizopo hivi sasa na hivyo kuwasaidia vijana wa kitanzania wanaojiunga na vyuo vikuu kuweza kusomeshwa.

"Ni vyema kwa wanufaika ambao tayari wana shughuli zinazowapatia kipato, kukumbuka kuhusu hili deni la mkopo wa HESLB, kujitokeza mapema na kuanza kurejesha ili fursa hiyo iwafikie watanzania wengi zaidi", anasisitiza Nanauka.

Kampeni ya 'Fichua' inalenga kuwahamasisha watanzania wazalendo kuwafichua watu mbalimbali wenye vipato na walionufaika na mikopo ya elimu ya juu lakini hawajaanza kurejesha mikopo yao, kujitokeza na kuanza kurejesha mikopo hiyo ili fedha zitakazokusanywa ziwezeshe watanzania wahitaji kusomeshwa elimu ya juu.

Njia mbalimbali za kuwafichua wanufaika ambao hawajaanza kurejesha zimekuwa zikitumika, ikiwemo watu wenye nia njema kuwasilisha taarifa zao kupitia barua pepe (info@heslb.go.tz), kwa njia ya simu (0736 665 533) au kufika ofisi za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu zilizopo Dodoma, Zanzibar, Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Mtwara ili kuwafichua wanufaika ambao wana shughuli zinazowapatia kipato lakini hawajaanza kurejesha.

Serikali imetoa TZS 7.2 Trilioni na kusomesha watanzania 754,000 kati ya mwaka 1994/1995 na sasa ambapo kiasi cha TZS 1.34 Trilioni zimeshakusanywa ikiwa ni 64% ya TZS 2.1 Trilioni zilizoiva zinazotakiwa kukusanywa na hivyo ipo haja ya kuhakikisha 36% iliyobaki pia inakusanywa ili kuufanya mfuko wa mikopo ya wanafunzi kuwa endelevu na stahimilivu.

**FICHUA**
**Barua Pepe:**
**info@heslb.go.tz**
**Simu:**
**0736 665 533**



# HESLB, WAHARIRI WAKUTANA KUTATHMINI MAFANIKIO

Na Mwandishi Wetu
Dar es Salaam

Menejimenti ya HESLB imekutana na wahariri kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini na kupata fursa ya kuzungumzia masuala muhimu ya Bodi ya Mikopo ikiwemo urejeshaji wa mikopo iliyoiva kutoka kwa wanufaika wake. Mkutano huo ulifanyika Alhamisi, Oktoba 26, 2023, katika Ukumbi wa PSSSF Golden Jubilee jijini Dar es salaam ambapo pamoja na mambo mengine HESLB ilipata nafasi ya kuwasilisha taarifa na kubadilishana mawazo na wahariri kuhusu safari ya mafanikio katika kipindi cha miaka minne iliyopita.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Abdul-Razaq Badru amesema katika kipindi cha miaka minne (2020/2021 – 2023/2024), Serikali imeongeza bajeti ya mikopo kwa asilimia 69… kutoka TZS 464 bilioni hadi TZS 786 bilioni.

"Ongezeko hili lina tija kwetu, lakini pia kwa wanafunzi tunaowahudumia na kwa ukubwa huo imewezesha ongezeko la idadi ya wanufaika kwa mwaka, kutoka 149,506 hadi 220,376 watakaonufaika mwaka huu wa masomo (2023/2024)," amesema Badru.

"Bajeti ya mkopo iliyotengwa mwaka huu ni TZS 786 bilioni, mikopo ya wanafunzi wa shahada ya kwanza (tengeo la TZS 731 bilioni), Samia Skolashipu (tengeo la TZS 6.7 bilioni) na mikopo kwa stahahada katika fani sita za kipaumbele (tengeo la TZS 48 bilioni) … ongezeko hili ni kubwa kuwahi kutokea ambalo limeenda sambamba na kutanua wigo wa utoaji mikopo kwa vyuo vya kati," amefafanua Badru.

Pamoja na mambo mengine, Badru alieleza mpango mkakati wa HESLB wa kuzindua kampeni ya #Fichua yenye lengo la kutoa hamasa kwa wadau wa elimu kufichua wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu wenye vipato ambao hawajaanza kurejesha mikopo hiyo.

Kuhusu suala la urejeshaji mikopo, Badru amesema kiasi cha TZS 530 bilioni kimekusanywa na kuwasilishwa katika kipindi cha miaka minne kati ya lengo la kukusanya TZS 565 bilioni kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo.

Mjumbe wa Kamati ya Tendaji ya Jukwaa la Wahariri (TEF), Neville Meena ameipongeza HESLB kwa namna inavyopambana katika utoaji huduma ili kuhakikisha wanafunzi wanatimiza malengo yao sambamba na kufikia ndoto zao.

"Kipekee nitoe pongezi zangu za dhati kwenu, hususani katika utoaji wa huduma! mmejiimarisha sana …tunao wanahabari waliopo katika vyombo mbalimbali vya habari ambao walinufaika na mikopo hii. Niwaahidi tutakuwa mabalozi wazuri wenye hamasa ya kuhakikisha wale ambao hawajarejesha bado wanarejesha ili na wengine wasome", amesema Meena.

Kwa kutambua umuhimu wa vyombo vya habari katika kuhabarisha, kufundisha na kuburudisha, Menejimenti ya HESLB inavitumia vyombo hivyo kama mdau muhimu wa ugharimiaji wa elimu ya juu na imekuwa na utaratibu wa kushirikiana kwa karibu ili kuwezesha utoaji sahihi na kwa wakati wa taarifa za mikopo ya elimu ya juu nchini.

HESLB
BODI YA MIKOPO
TUNAWEKEZA KWA KIZAZI CHA BAADAE



# SAMIA SCHOLARSHIP 2023/2024

### SIFA ZA KUPATA UFADHILI
- Awe Mtanzania;
- Awe na ufaulu wa juu kwenye mtihani wa taifa ya kidato cha sita mwaka 2023 iliyoendeshwa na NECTA katika tahasusi za sayansi;
- Awe amepata udahili katika Chuo cha Elimu ya Juu hapa nchini kinachotambuliwa na Serikali katika programu za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati au Tiba
- Awe ameomba ufadhili kwa usahihi kwa njia iliyoelekezwa. https://olas.heslb.go.tz

### MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA:
- Ufadhili huu ni wa asilimia mia moja ambao kikomo chake kitazingatia miongozo ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.
- Orodha ya majina ya wanafunzi husika inapatikana kupitia www.moe.go.tz na www.heslb.go.tz

- Ni kwa masomo ya shahada ya kwanza kwa wanafunzi waliopata ufaulu wa juu katika mitihani ya Kidato cha Sita mwaka 2023
- Mitihani iliyoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) katika Tahasusi za Sayansi (PCB, PCM, PGM, CBG, CBA, PMC na CBN).
- Itagharimia kwa asilimia mia moja (100%) masomo ya Elimu ya Juu kwa wanafunzi 640 ambao wamepata udahili katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati na Tiba mwaka huu 2023/2024.

HESLB Tanzania HESLB Tanzania HESLB_Tanzania

**#Kazilendelee**
**#WeweNdoFuture**
**#TimizaWajibu**

## DODOMA

Jengo la PSSSF, Br. Makole, eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma
+255 758 067577
+255 739 067577
dodoma@heslb.go.tz

## HUDUMA KWA WATEJA

PSSSF Twin Tower
Ghorofa ya chini
Mtaa wa Misheni
S.L.P 76068,
Dar es Salaam
Simu: +255 758 067 577
+255 739 067 577
Email: info@heslb.go.tz

## DAR ES SALAAM

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu
1 Mtaa wa Kilimo, Tazara,
Br. Mandela
S.L.P 76068, 15471
Dar Es Salaam
Simu: 0736 665 533
Email: info@heslb.go.tz

## ZANZIBAR

Jengo la Michenzani Mall,
Eneo la Michenzani
Ghorofa ya Tano
S.L.P 900, Zanzibar,
Simu: 0779 321 424
Email: zanzibar@heslb.go.tz

## ARUSHA

NSSF Jengo la Mafao,
Ghorofa ya Kwanza
S.L.P 2712, Arusha
Simu: 027 2520128
0624 100 011
0739 102 016
Email: arusha@heslb.go.tz

## MWANZA

PSSSF Plaza, ghorofa ya pili
Br. Kenyatta
S.L.P 3051, mwanza
Simu: 028 2506008
0759 819 350
0738 153 661
Email: mwanza@heslb.go.tz

## MBEYA

Jengo la CAG, Br. Mbalizi
S.L.P 319, Mbeya
Simu: 0738 131 310
0738 131 311
Email: mbeya@heslb.go.tz

## MTWARA

NHC Raha Leo Complex,
Ghorofa ya pili
S.L.P 969, Mtwara
Simu: 0733 068 171
Email: mtwara@heslb.go.tz